# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 50 Ufalme wa Mungu

**SOMA** **Mathayo 24:36 – 44; Zekararia 14:2 – 4; Zaburi 2;
Danieli 12:1 – 3; 2 Wakorintho 5:10; Isaya 11:1 – 9; Isaya 35**

**SOMO**

Yesu alifundisha wanafunzi wake kuomba hivi, “Baba yetu uliye Mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko Mbinguni …” Mungu ameahidi kwamba Yesu atakuja kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. Mungu anataka dunia ijazwe na watu wanaompenda na wawe wake kama wanawe. Anataka kuondoa laana duniani na kuwe na vyakula vingi vya kutosha kila mtu. Anataka kuondoa kifo ili watu waishi milele. Hii ndiyo maana ya Mapenzi ya Mungu yatimizwe hapa duniani. Hii itafanyika wakati Yesu atarudi kutoka Mbinguni ili asimamishe Ufalme wa Mungu hapa duniani.

Kuna ishara nyingi hapa duniani za kuonyesha kwamba Yesu yuko karibu kuja. Hatujui tarehe atakayekuja. Lakini tunajua kwamba kuja kwake kuko karibu. Yesu alitwambia, “Tukeshe … lazima uwe tayari kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja wakati hatumtarajii.” Lazima tuwe tukikesha tukimwongojea hali tunaishi maisha ya upendo na tuwe na imani tukimtii Mungu. Kila asubuhi tukiomba kwamba Yesu akuje leo. Tukiishi, tuishie Mungu sasa hatuna siku ingine iliyobaki.

Yesu alisema kwamba dunia itakuwa na uovu sana wakati ya kurudi kwake. Aliilinganisha na wakati wa Nuhu, dunia ilikuwa mbaya sana mpaka Mungu akaiharibu. Watu watakuwa na haja ya maisha yao wenyewe - wakinunua, wakiuza, wakila, wakinywa, wakioana n.k. Hawatakuwa na wakati na Mungu kabisa. Hivyo ndivyo dunia yetu imefikia sasa. Imekuwa muovu sana. Watu hawana haja na Mungu katika maisha yao. Kuna ujeuri na uzinzi mwingi. Serikali ina ufisadi na ulafi mwingi. Mungu atahukumu ulimwengu, wakati Yesu atarudi. Kutakuwa na wakati wa hukumu dunia ya uovu kabla Ufalme wa Mungu wa Amani uanze.

Karibu kila siku taifa la Israeli linakuwa kwa habari. Israeli imezungukwa na maadui. Hivi karibuni, hawa maadui wote watawashambulia. Mungu atatokezea na kuokoa watu wake. Mungu atatuma Yesu kuja kuharibu maadui wa Waisraeli na atakuwa Mfalme.

**Maswali na Majibu**

*1.* Ulimwengu utakuwa wa namna gani Yesu atakaporudi?
*Utakuwa muovu sana, watu wengi hawatakuwa na haja na Mungu.*

*2.* Yesu atafanya nini baada ya kufufua wafu?
*Atahukumu watu.*

*3.* Uzima wa milele ni wa namna gani?
*Kuishi milele, kwa amani na ushirika na Mungu, bila maumivu, dhambi au mateso.*

4. Aina ya watu gani wawili wataishi kwa Ufalme wakati wa Yesu?
*Watu wakukufa na watu walio na uzima wa milele*.

*5.* Watu wanaokufa watafanya nini?
*Wataishi vile tunaishi sasa – wafanye kazi, wazae watoto, wafanye dhambi na wakufe.*

*6.* Watu wasiokufa watafanya nini?
*Watasaidia Yesu kutawala ulimwengu na wafundishe na kusaidia watu.*

*7.* Ukulima utakuwa tofauti namna gani kwa Ufalme?
*Hakutakuwa na makwekwe n.k. mvua itakuwa nyingi na mavuno mazuri.*

*8.* Nini itafanyika kwa wagonjwa na walemavu? *Wataponywa.*

*9.* Watu wasiokufa watafundisha watu nini?
*Kuhusu Mungu na sheria zake za haki.*

*10.* Kutakuwa na vita wakati wa Ufalme?
*Hapana. Kutakuwa ni wakati wa furaha na amani na watu watapenda Mungu na kutii sheria zake.*

### Mistari ya kukariri

2 Wakorintho 5:10 Danieli 12:1 – 3 Isaya 35:5 – 6

### Mazungumzo

.Zungumzia nini itafanyika Yesu atakaporudi hapa duniani. Ulimwengu utakuwa tofauti namna gani na wakati wa sasa?

### Kuandika

Andika juu ya eneo ya ulimwengu yenye utaenda kusaidia Kristo kama mmoja wa watu wasiokufa. Utasaidia watu wa huko namna gani?

Mataifa mengi yatakuja kupigana na Waisraeli na Yerusalemu. Lakini Yesu atarudi kuwaharibu. Vile atatua kwa Mlima wa Mizeituni, kutakuwa na mtetemeko mkubwa wa nchi na uharibifu mbaya sana. Yesu atarudi kwa nguvu na utukufu mkuu kuhukumu wale wanaoasi na kushambulia watu wa Mungu. Mataifa mengine hawatakubali Yesu kama Mfalme wao. Watamkataa. Watakaomkataa watahukumiwa na kuharibiwa.

Yesu atakaporudi, atafufua wafu kuwa hai tena. Na kuwasanya pamoja watakao kuwa hai. Wote watasimama mbele ya kiti cha hukumu na wahukumiwe kulingana na vile waliishi maisha yao. Walioishi maisha ya imani watapewa miili ya maisha ya milele na watasaidia Yesu kutawala nchi. Waovu wataadhibiwa na kuharibiwa milele. Wataondolewa kwa Ufalme wa ajabu wa Mungu.

Kitabu cha Ufunuo kinatusaidia tuelewe vile Yesu atatoa hukumu. Ufunuo inatwambia juu ya kitabu cha Uzima. Ni kama Mungu anaweka kitabu cha ukumbusho. Baada ya kubatizwa Mungu anaandika jina la mtu juu ya ukurasa. Kila wakati ukifanya jambo lolote, liwe mbaya au mzuri, inaandikwa kwa ukurasa wake. Wakati Yesu atakuwa akihukumu, ataangalia kwa huo ukurasa. Mungu hawezi kuweka makosa ikae milele. Kwa hivyo Yesu atafuta mabaya yote tuliyofanya ikiwa tutakuwa na msamaha. Baadaye ataangalia ni nini imebaki. Lakini yaliyobaki yawe ni makosa tu, hatutapewa uzima wa milele, tutaharibiwa. Ikipatikana tuna ukumbusho wa mazuri, tutapewa uhaki kwa kuongezewa mazuri kwa huo ukurasa na kupata uzima wa milele.

Uzima wa milele ni uzima wa kipekee. Ni uzima usio na mwisho, ni kuishi kwa ajabu, yaani zaidi ya kuishi. Wale watakaopata huu uzima, hawatatenda dhambi tena. Watakuwa na amani ya ajabu na ushirika na Mungu na Bwana Yesu. Tabia zao zitakuwa kama za Yesu. Watakuwa na akili na hekima ya juu. Hawatakuwa na huzuni wala uchungu.

Yesu atakuwa Mfalme kule Yerusalemu. Yerusalemu ni mji uliochaguliwa na Mungu uwe mji mkuu. Hii itatimiza ahadi kwa Daudi kwamba Masiya atatawala kutoka kwa kiti chake cha enzi. Yerusalemu iko katikati ya dunia. Huu utakuwa mwanzo wa mpango mpya wa utawala wa ulimwengu wa Yesu kama mtawala wa haki, kweli na sawa kutoka Yerusalemu.

Yesu atatawala na sheria za Mungu. Zitakuwa sheria za kweli. Hakutakuwa na ufisadi. Yesu atakuwa na mamlaka na nguvu za kuwezesha hizo sheria. Sheria za Mungu zitaleta amani na haki ulimwenguni. Hakutakuwa na vita tena.

Watu wasiojua habari ya Injili, Yesu atakaporudi, hawatasimama mbele ya kiti cha hukumu. Wataendelea kuishi kwa Ufalme, kama watu wa kawaida. Watafanya kazi, watazaa watoto, waishi na kukufa vile tuko saa hii.

Kwa hivyo tutakuwa na watu aina mbili kwa Ufalme wa Mungu. Kutakuwa na wale wenye wameenda kwa kiti cha hukumu na kupewa uzima wa milele. Na kutakuwa na wale wasiojua Injili. Watakaa na kuishi kama watu wa kawaida kwa Ufalme.

Watu wa miili isiyokufa (waliofaulu), watakuwa watawala tena walimu kwa huo Ufalme wa ulimwengu mzima wa Mungu. Yesu atawatuma ulimwenguni kote kwa eneo yenye watatawala na kufundisha. Itachukuwa muda mrefu kufundisha neno la Mungu hawa watu wanaokufa na kuzuluhisha shida zao za kawaida. Itakuwa kazi ya ajabu ya kusaidia Yesu kulainisha kila kitu hapa duniani. Ufunuo inatwambia itachukuwa miaka 1,000.

Wakati Yesu atakuwa Mfalme Yerusalemu, watu hawatajua haraka kuhusu Mungu na sheria Zake. Itakuwa wajibu wa hawa watu walio na miili isiyokufa kusaidia Yesu kwa hizo eneo zenye amawapea kuwafundisha juu ya Mungu na Ufalme Wake wa ajabu. Mwishowe ulimwengu wote utajua Injili. Dunia itakuwa pahali pazuri zaidi, pafuraha na hata walio na miili ya kufa watafurahia baraka kwa Ufalme wa Mungu.

Mungu ataondoa laana yenye aliweka wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi. Kutakuwa na mvua na mimea ya kutosha kila mwaka. Kila mtu atakuwa na chakula cha kutosha. Watu watakuwa wa nguvu na afya nzuri. Wasaidizi wa Yesu walio na miili isiyokufa, watakuwa na uwezo wa kuponya , vile Yesu alikuwa akifanya wakati alikuwa hapa duniani. Wataponya vipofu na viziwi, viwete na bubu. Hospitali haitakuwa na wagonjwa sana. Hebu jiangalie ni furaha namna gani kuwa wewe ndiye uliye na hayo mamlaka ya kuponya wanaoteseka hospitalini.

Kwa Ufalme kutakuwa ni wakati wa amani na haki, wakati wa furaha na wingi wa mazuri. Watu ulimwenguni kote watajifunza juu ya Mungu na njia Zake. Watasafiri kwenda Yerusalemu kuabudu Yesu kama Mfalme.

Mungu anataka tuwe kwa Ufalme Wake. Ametuchagua sisi tusaidie Yesu kutawala ulimwengu. Tunatakiwa tuanze sasa kujifunza. Tunatakiwa tusonge karibu na Mungu na tukue na tabia za Yesu. Tunatakiwa tufunze watu juu ya Mungu na tusaidie walio na shida. Hebu tuombe, “Ufalme Wako uje, Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani."